# MKATABA WA UPANGAJI OFISI YA BIASHARA

MWENYENYUMBA: COSMOS CONSTRUCTIO LIMITED

MPANGAJI: MELAKA OIL TANZANIA LIMITED

# MKATABA WA UPANGAJI NYUMBA YA OFISI YA BIASHARA

Mkataba huu umetayarishwa leo tarehe ........02........./..........01........../ 2023

**Mkataba wa upangaji umefanyika leo tarehe MKATABA HUU** umefanyika leo tarehe .......02........ / ...............01............ / 2023 baina ya **COSMOS CONSTRUCTION LIMITED S.L.P. 12288** Dar es salaam; (ambaye katika mkataba huu atajulikana kama **"Mwenyenyumba"** kwa upande wa kwanza) na **MELAKA OIL TANZANIA LIMITED** ya S.L.P 12288, Dar es salaam; (ambaye katika mkataba huu atajulikana kama **"Mpangaji"** kwa upande wa pili);

**Kwa kuwa Mwenyenyumba** anamiliki Nyumba na. 16 iliyopo ndani ya kiwanja na. 77, kitalu na. A, Barabara ya Siwa, eneo la Mikocheni Light Industrial, Kata ya Mikocheni, Wilaya ya Kinondoni, Dar es Salaam na ameamua kumpangisha **Mpangaji** kwa makubaliano kama yanavyoonekana hapo chini. Na kwa upande wa pili **Mpangaji** ameiona sehemu husika na ameridhia kupanga kwa madhumuni ya kufanya Ofisi ya biashara.

<u>MTABA HUU UNASHUHUDIA MAKUBALIANO YAFUATAYO</u>

1. Muda wa pango ni miaka mitatu (3) tu kuanzia tarehe .........02......... / ..........01.............. / 2023 mpaka ......01..........Mwezi.........01..........2026.
2. Kodi ya mwezi ni sh Shillingi Milioni Tano na Laki Tano tu (Tshs. 5,500,000/=) na **Mpangaji** tayari amelipa jumla ya Shillingi za Kitanzania Milioni Sitini na sita tu (Tshs. 66,000,000/=) ikiwa ni kodi ya mwaka mmoja, wakati wa kusaini mkataba huu na **Mwenyenyumba** anakiri kupokea kiasi hicho cha fedha.
3. Kwamba kodi italipwa kwa awamu tatu yaani kila mwaka mpaka mkataba utakapoisha katika mfumo wa fedha taslimu.
4. Kwamba **Mpangaji** atazingatia sheria, kanuni na taratibu zote za upangaji.



CamScanner

5. **Mpangaji** atatumia eneo husika kwa shughuli za kufanya Ofisi ya biashara tu. Pia **Mpangaji** anatakiwa kuhakikisha ulinzi na usalama wa mali zake katika kipindi chote cha mkataba.
6. **Mpangaji** hatakiwi kufanya matengenezo yoyote bila kibali cha **Mwenyenyumba**, **Mpangaji** atafanya ukarabati mdogo wakati ukarabati mkubwa utafanywa na **Mwenyenyumba**.
7. **Mpangaji** atatakiwa kulipa kodi ya pango kwa wakati muafaka.
8. Malipo ya umeme na maji ni juu ya **Mpangaji**.
9. **Mpangaji** atatakiwa kuhakikisha nyumba na mazingira yake yanakuwa safi muda wote na atawajibika kuchangia ada ya usafi wa mazingira ya pamoja atakayokubaliana na **Mwenyenyumba** katika kipindi chote cha mkataba huu.
10. **Mpangaji** hataruhusiwa kupangisha mtu mwingine ofisi hiyo bila ridhaa ya **Mwenyenyumba.**
11. Notisi ya mwezi mmoja kwa kusudio la kuvunja mkataba, inaweza kutolewa na upande wowote wa mkataba huu.
12. **Mpangaji** atatakiwa kutoa notisi ya mwezi mmoja kabla ya Mkataba huu kwisha endapo atakua na nia ya kuendelea na mkataba kwa mwaka mwingine kwa masharti yatakayokubalika kwa wakati huo.
13. Endapo **Mwenyenyumba** hatakua na nia ya kumpangisha tena **Mpangaji** atawajibika kutoa notisi ya siku 30 kwa **Mpangaji** ya kuhama kwenye ofisi.
14. Mkataba huu utaongoza na Sheria za Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.

1. **MWENYE NYUMBA** amekubaliana na **MPANGAJI** kama ifuatavyo:

   a) **Mwenyenyumba** atalipa kodi zote za serikali, kama kodi ya ardhi na majengo, na atawajibika na uharibifu wowote utakaosababishwa na majanga ya asili,na wakati huo kodi itakua imesitishwa hadi matengenezo yatakapokua yamekamilika.

   b) **Mpangaji** ambaye amelipa kodi na anatekeleza masharti yaliyoainishwa katika mkataba huu, ataitumia **Ofisi** bila bugudha na usumbufu wowote kutoka kwa **Mwenyenyumba** au mtu mwingine yoyote au mtu ambaye ameidhinishwa na **Mwenyenyumba**.



CS CamScanner

**KWA KUSHUHUDIA MKATABA HUU** pande zote mbili zimeweka sahihi katika tarehe na siku kama inavyoonekana hapa chini:-

**UMETIWA SAHIHI na KUTOLEWA** Dar es Salaam na kwaniaba ya **COSMOS CONSTRUCTION LTD** leo hii tarehe ...02...mwezi ......01..........2023 } ..........................
**MWENYE NYUMBA**

**JINA:** SIMON MOGAMBI MOREKA
**SAHIHI:** ____________
**CHEO:** GENERAL MANAGER
**ANUANI:** BOX 12288 DAR ES SALAAM

**MBELE YANGU;**
**JINA:** BORA ALFREDY NICHOLAUS
**SAHIHI:** ____________
**CHEO:** WAKILI
**ANUANI:** S.L.P 34674, DAR ES SALAAM

BORA ALFREDY NICHOLAUS Advocate, Notary Public & Commissioner for Oaths P.O. Box 34674, D.S.M

**UMETIWA SAHIHI na KUTOLEWA** Dar es Salaam na kwaniaba ya **MELAKA OIL TANZANIA LIMITED** mbele yetu leo hii tarehe ...02... Mwezi ...01.........2023 } ..........................
**MPANGAJI**

MELAKA OIL TANZANIA LIMITED P. O. Box 12288 DAR ES SALAAM

**JINA:** KHALED MOHAMMED BAKHORAH
**SAHIHI:** ____________
**CHEO:** DIRECTOR
**ANUANI:** S.L.P 12288, DAR ES SALAAM

**MBELE YANGU;**
**JINA:** BORA ALFREDY NICHOLAUS
**SAHIHI:** ____________
**CHEO:** WAKILI
**ANUANI:** S.L.P 34674, DAR ES SALAAM

BORA ALFREDY NICHOLAUS Advocate, Notary Public & Commissioner for Oaths P.O. Box 34674, D.S.M



CamScanner